**HALMASHAURI YA WILAYA YA __________, SHULE YA MSINGI ___________**
**MTIHANI WA UPIMAJI, DARASA LA IV.**
**SOMO : HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

**Muda: saa 1:30** **2025**

## SEHEMU A (Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Jibu vipengele (i) - (x) kwa kuchagua jibu sahihi na kuandika **herufi yake** katika kisanduku ulichopewa.

**(i)** Shughuli za kijamii zilitumika kuwaelimisha wanajamii kuhusu umuhimu wa kushikamana na maadili A.jando na unyago B. Matambiko na Sherehe C.Shule na majukwaa D.shule na makanisa

**(ii)**________yalichukua nafasi muhimu katika sayansi na teknolojia ya tiba za asili, yakiwa msingi wa usalama, siri, na ufanisi wa tiba A.maadili B. mila na desturi C. Maarifa D. Maisha [ ]

**(iii)** katika jamii za kale Vyanzo vya dawa vilipatikana kwa urahisi kutoka wapi?
A.Mazingira ya asili B. hospitalini C. Kwenye maabara za jamii D.Famasi za kale [ ]

**(iv)** Ipi kati ya zifuatazo ni Sayansi na Teknolojia Zilizotumika Kutengeneza Dawa?
A.kuchoma B.kupima kwenye maabara C.Kuyeyusha D. Kujenga bohari za madawa [ ]

**(v)** Taja rasilimali za asili zilizotumiwa na Jamii za kale kutengeneza nguo?
A. ngozi za wanyama na magome ya miti B. Pamba na magome ya miti C. Ngozi za Wanyama na pamba D. Majani ya mime na pamba [ ]

**(vi)** Ni jamii zilizokuwa Maarufu kwa nguo zao za mbungu A. wachaga. B. Wahaya . C. wanyamwezi D. wasukuma [ ]

**(vii)** uliwezesha utengenezaji wa zana bora za kilimo, uwindaji, na uvuvi. Hii ilisababisha uzalishaji mkubwa wa mazao na mazao ya baharini.. A. zana za chuma B.Zana za kati C.Zana za mawe D.Zana za kale [ ]

**(viii)** Ni shughuli ya kiuchumi muhimu kwa jamii za kale zilizokuwa karibu na bahari, maziwa, na mito mikubwa. A. Kilimo B. uvuvi C. Utalii D. Usafirishaji [ ]

**(ix)** Walitoka Kaskazini mwa Ziwa Nyasa na walitengeneza vyombo imara
A. wakisi B. wapare C. wachaga D.wafipa [ ]

**(x)** Walikuwa maarufu kwa kutengeneza nyavu na mitego
A. Wanyina B. wandali C. wajita D.wahehe [ ]

2. Jibu vipengele (i) – (v) kwa kuoanisha Orodha A na Orodha B. maelezo kuhusu Vichocheo vya mabadiliko ya sayansi na teknolojia kabla ya ukoloni.

| Orodha A | Herufi | Orodha B |
|---|---|---|
| **(i)** ni mwenendo au utendaji uliokubalika katika jamii. | ( ) | A Elimu ya jando na unyago |
| **(ii)** ilihusisha mafunzo maalum kwa vijana waliokuwa wanakaribia balehe. Mafunzo haya yalikuwa muhimu kwa jamii kwa sababu yaliwaandaa vijana | ( ) | B Vifaa vya jadi zilizotumika katika ujenzi<br>C Elimu ya jadi |
| **(iii)** sehemu ambapo jamii huishi na kufanya shughuli zao za kila siku. Kabla ya ukoloni, makazi ya jamii zetu yalitegemea mambo kadhaa muhimu;. | ( ) | D Mabadiliko ya kidemografia<br>E Wangoni na wanyakyusa<br>F makazi |
| **(iv)** Udongo, nyasi, miti, na mawe.. | ( ) | G Maadili |
| **(v)** walijenga nyumba kubwa kwa wazazi na ndogo kwa vijana wa kiume. | ( ) | H Mahitaji ya kijamii |

3. Jibu vipengele **(i) - (v)** kwa kuchagua jibu sahihi katika sanduku hapo chini na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

| |
|---|
| Uaminifu, Heshima, ukweli, Utu, upendo, umoja, ushirikiano |

i) Thamani ya binadamu inayojumuisha huruma, ukarimu, na heshima huitwa________
ii) Kuonyesha adhimu kwa haki na maoni ya wengine huitwa______________________
iii) Kujali na kuonyesha huruma kwa wengine kwa dhati huitwa____________________
iv) Hali ya kusema na kutenda kwa usahihi na uwazi huitwa________________________
v) Kuwa na tabia ya kuaminika na kutimiza ahadi huitwa__________________________

**SEHEMU B (Alama 18)**

4. jibu maswali katika vipengele (i) - (iii):

(i) Taarifa za kihistoria ni muhimu kwetu, kwa jamii na Taifa. Hivyo, kujifunza historia ya Tanzania ni muhim. Taja faida mbili za kujifunza historia ya Tanzania na maadili
a. ____________________________________ b. _______________________________.

(ii) Taja vitendo viwili vya kimaadili vinavyoonesha heshima vinavyofanyika shuleni
a. _________________________________ b. _________________________________

(iii) Kwanini vitendo vya kimaadili ni mhimu katika jamii yoyote (taja umhimu mmoja)________

5. Chunguza kwa makini picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.



**Maswali**

**(a)** Taja shughuli iliyokuwa ikifanywa na jamii za kale kujipatia chakula iliyoonyeshwa katika picha hapo juu? __________________________________________

**(b)** Taja vifaa viwili vilivyokuwa vikitumika katika shughuli iliyoonyeshwa hapo juu kwenye picha
a)_____________________________________ b) _____________________________

**(c)** Eleza faida moja ya shughuli uliyotaja swali (i) katika jamii za kale ________________

**(d)** Ni Wanyama gani walitumika katika shughuli uliyotaja swali (i) katika jamii za kale? _____

**(e)** Taja vifaa viwili vilivyokuwa vikitumika katika shughuli hiyo iliyoonyesha kwenye picha hapo juu. i. __________________________________ ii____________________________

**SEHEMU C (Alama 12)**

Jibu swali la **sita (6)**

6. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali katika vipengele (a) – (f) kwa kuandika jibu lililo sahihi katika sehemu zilizoachwa wazi.

Tanzania ni nchi iliyopatikana baada ya kuunganishwa kwa Tanganyika na Zanzibar mnamo tarehe 26 Aprili 1964 Tanganyika ilipata uhuru wake kutoka kwa Waingereza tarehe 9 Desemba 1961, na Zanzibar ilipata uhuru tarehe 10 Desemba 1963, kisha mapinduzi yalifanyika Januari 1964. Viongozi waliokuwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru walikuwa kama Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa Tanganyika na Sheikh Abeid Amani Karume wa Zanzibar.

Baada ya uhuru, serikali iliweka mkazo mkubwa katika kuhimiza umoja, amani, na maadili mema kwa wananchi. Maadili hayo yalijumuisha heshima kwa wakubwa, kushirikiana, ukweli, na uzalendo. Mwalimu Nyerere alisisitiza falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea, akiamini kwamba maendeleo ya kweli yanatokana na mshikamano wa wananchi.

Mpaka leo, historia ya Tanzania inafundisha umuhimu wa maadili mema kama msingi wa jamii yenye maendeleo na mshikamano. Vijana wanafundishwa kuenzi historia hii kwa kuwa waadilifu, watiifu, na wazalendo.

**MASWALI**

i. Tanzania ilianzishwa rasmi tarehe ngapi?__________________________________
ii. Ni viongozi gani wawili waliotajwa kama wapigania uhuru katika kifungu? ___________________
iii. Maadili gani yalihimizwa baada ya Tanzania kupata uhuru? Taja angalau mawili
a. ___________________________________ b)______________________________________
iv. Kwa nini ni muhimu kwa vijana wa leo kuenzi historia ya Tanzania? ______________________

**KWA MAHITAJI YA EDUCATIONAL SUPPORT SERVICES KAMA MAAZIMIO, MAANDALIO, MITIHANI, NUKUU ZA SOMO, VITABU N.K (KUANZIA WALI HADI KIDATO CHA SITA)**

# WASILIANA NASI:

## MBI EDUCATIONAL SERVICES AND STATIONERY

**KUPITIA:**

**CALL, MESSAGE OR WHATSAPP:**

# 0766617162
# 0683205565

**EMAIL:** info@mbieducationalservices.co.tz
**WEBSITE:** https://mbieducationalservices.co.tz

I. **MITIHANI KWA KILA SETI YA SHULE ZA MSINGI (BOTH SWAHILI AND ENGLISH MEDIUM SCHOOLS) NI SH. 8000, KILA SOMO O'LEVEL NI SH. 2500, KILA SOMO A'LEVEL NI SH. 3000 TU**

II. **KILA AZIMIO MSINGI SH. 1500, O'LEVEL SH. 2000, ADVANCE 3000 TU KWA KILA SOMO**

III. **NUKUU ZA SOMO NI SH. 5000 KWA KILA SOMO (AWALI, MSINGI NA O'LEVEL), NI SH. 10000 KWA KILA SOMO (A'LEVEL)**

IV. **MAANDALIO YA SOMO (MSINGI SH. 8000 KILA SOMO), (O'LEVEL SH. 5000 KILA SOMO), (A'LEVEL SH. 10000 KILA SOMO)**

# LIPIA KUPITIA:

**VODACOM LIPA NAMBA: 58151873**
**Jina: MBI EDUCATIONAL SERVICES AND STATIONERY**

**YAS/TIGO LIPA NAMBA: 15049263**
**Jina: MBI EDUCATIONAL SERVICES AND STATIONERY**

**AIRTEL LIPA NAMBA: 13355758**
**Jina: MBI EDUCATIONAL SERVICES**

**HALOTEL LIPA NAMBA: 23450919**
**Jina: MBI EDUCATIONAL SERVICES**

**NMB ACCOUNT: 51610090884**

**Jina: MBI EDUCATIONAL SERVICES AND STATIONERY**

**UKINUNUA AZIMIO, ANDALIO AU MITIHANI UTAPATA OFFER YA KUJAZIWA TAARIFA ZAKO KAMA UKIHITAJI, KAMA VILE:**

- **Jina la halmashauri shule ilipo**
- **Jina la shule**
- **Jina la mwalimu**
- **Darasa na mkondo**
- **Nembo ya halmashauri shule ilipo**
- **Nembo ya shule kama unayo**
- **Picha yako/ya shule/ darasa n.k, kama ukihitaji ionekane kwenye cover page**